

Ushuhuda

NANI ANAKWENDA MBINGUNI?

Nani anakwenda mbinguni? Na pia nani anakwenda jehanum? Hayo ni maswali muhimu kwa Wakristo na Waislamu pia. Mwenye dhambi aliyesamehewa anakwenda mbinguni. Lakini Mwislamu je? Ndugu aitwaye Isaka, aliyekuwa Mwislamu zamani, kwa hakika anakwenda mbinguni wala hataki kuwaacha wengine nyuma. Yafuatayo ni ushuhuda wa Isaka.

Ingawa nililelewa katika familia ya Kiislamu yenyeye maadili makali, nilisoma katika shule ya Kanisa la Uganda (Anglikana) ambapo nilianza kujifunza habari za Yesu. Kutokana na uhusiano huo na Wakristo, nilitambua kwamba kuna aina mbili za ujumbe zisizokubaliana kuhusu uzima wa milele. Mawazo ya watu wengi ni kwamba wale wasiovuta sigara, kunywa pombe, kuiba na kadhalika, watakwendwa mbinguni. Kwa upande mwingine, ujumbe wa Biblia ni kwamba Yesu peke yake anasamehe dhambi, na kwamba Yeye ndiye njia iendayo uzima wa milele (Yohana 3:16, 14:6).

Nilipoendelea kufahamu tofauti ya aina hizo mbili za ujumbe, mvutano ulianza ndani yangu. Kufuatana na kipimo cha kibinadamu, hakika nilikuwa mtu mwema, kwa sababu sikuvuta wala kulewa. Lakini nilipojifunza zaidi kutokana na Maandiko Matakatifu, nilifahamu kwamba kila mtu ni mwenye dhambi, mlevi pamoja na "mtu mwema". Warumi 3:23 ni mstari unaohakikisha hali hiyo: "Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu".

Lakini ingawa Biblia ilinipatia ujumbe halisi kuhusu ni nani aendaye mbinguni na nani aendaye jehanum, bado niliogopa kuacha dini ya Uislamu. Akili yangu ilisumbuliwa na mawazo kuhusu maoni ya wazazi wangu, kama ningeweza kupata kazi na kujitegemea, na kama ningekubaliwa na Wakristo wengine. Mara nyingine niliogopa kwamba Waislamu wangejaribu kuniua kama ningeamua kuwa Mkristo.

Hatimaye nilianza kuhudhuria katika kanisa ambapo nilipata mafunzo zaidi ya Biblia. Mwaka uliofuata baba yangu alishindwa kulipa ada yangu ya shule, kwa hiyo nilikwenda kukaa nyumbani kwa Mkristo fulani. Pale ndipo niliposema wazi kwamba nilimwamini Yesu Kristo. Nilichukiwa na watu wengine kutokana na uamuzi huo, lakini Bwana alinilinda nao. Sasa nilikuwa katika njia iendayo mbinguni.

Baadaye nilipokuwa nikisoma Chuoni, nilikutana na wanafunzi wengi waliojihesabu Wakristo. Siku moja rafiki yangu mmoja alinionyesha picha ya msichana aliyempenda, akibusu picha hiyo kwa upendo. Nilipatwa na hisia ya kutamani kuwa na msichana pia, ili kuthibitisha kwamba nilipendwa na wasichana. Lakini zaidi nilivytamani sifa hiyo, zaidi upendo wangu kwa Yesu.

ulivyopungua. Lakini, Mungu asifiwe, Yesu alinipenda mpaka asiweze kuniacha nianguke na kumwacha. Ndipo tarehe 18 Machi 1967 nilipohudhuria mukutano wa uamsho, niligundua jinsi nilivyokuwa nimetembea mbali na Bwana nikajitoa Kwake kwa upya.

Tangu siku hiyo, nimepata furaha kuu katika kumtumikia Bwana wangu. Baada ya kuoa na kufanya kazi kama mwalimu, nimeona mzigo mkubwa moyoni mwangu kwa ajili ya Waislamu waliopotea katika eneo la nyumbani kwangu nchini Uganda. Mwaka 1988 chama cha uinjilisti kilianzishwa kwa ajili ya kuwatangazia wengine ujumbe wa Yesu Kristo uletao uzima. Leo sina mashaka yoyote kwamba ninakwenda mbinguni. Na hamu yangu ni kuwakaribisha Waislamu wengi iwezekanavyo wafuatane nami.